



**Na Rais Henry B. Eyring**  
Mshauri wa Pili katika Urais wa Kwanza

## Yesu Kristo yu Hai

**K**ipindi hiki cha mwaka khusaidia tukumbuke dhahibu ya Mwokozi na ufufuko Wake kutoka kaburini.

Niliwahi kusimama na mke wangu nje ya kaburi huko Yerusalemu. Ndani, tuliona benchi la jiwe kwenye ukuta.

Lakini taswira nyingine ikaja akilini mwangu. Nikamfikiria Mariamu hapo kwenye kaburi tupu. Alikuwa akilia kwa sababu Mwokozi alikuwa amekufa. Hakujuu pale ulipokuwa mwili Wake.

Kisha “akageuka nyuma, akamwona Yesu amesimama, asijue ya kuwa ni Yesu” (Yohana 20:14). Mariamu alidhani Yeye alikuwa mtunza bustani.

“Yesu akamwambia, Mariamu” (Yohana 20:16). Sasa Mariamu akamjua Yeye. Alijua Yeye Alikuwa amefufuka.

Kwa sababu Yesu Kristo alishinda kifo, watoto wote wa Baba wa Mbinguni wanaozaliwa duniani watafufuka katika mwili ambao kamwe hautakufa.

Ninamshukuru Baba yetu wa Mbinguni kwa ajili ya Zawadi ya Mwanawe Mpendwa. Nina shukrani kujua kwamba Yeye alifanya upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu na kufufuka katika ufufuko. Nashuhudia kuwa Yesu ni Kristo aliyefufuka, Mwokozi wetu na mfano wetu kamili. ●


Ilitoholewa kutoka “Roho Wake awe Nanyi,” *Liahona*, Mei 2018, 86–89 na “He Is Risen,” *Liahona*, Aprili 2013, 4–5.

## Hadithi ya Pasaka



## Hadithi ya Gurudumu la Pasaka

Kata miduara na uweke duara la kwanza juu ya jingine. Toboa shimo katikati na uzishikamanishe kwa pini au msumari bapa wa chuma. Kisha geuza mzunguko wa juu ili kusimulia hadithi ya Pasaka.



VIELEZO NAALYSA TALLENT